



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA KAKONKO



Simu Na. +255(028) 2820137
Fax Na. +255(028) 2820137
E-mail.ded@kakonkodc.go.tz
Tovuti: www.kakonkodc.go.tz

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji,
S.L.P 03,
KAKONKO.

Unapojibu tafadhali taja:
Kumb.Na. HW/KNK/S. 40/VOL. II/31

17.07.2023

YAH: TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kakonko anayo furaha kutangaza nafasi 4 za ajira ya kudumu kwa watanzania wote wenye sifa stahiki kwa nafasi ya **dereva daraja la II nafasi 4**. Nafasi za ajira hizi zinatokana na kibali cha Ajira kutoka kwa **Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala bora** kwa barua yenye Kumb. Na. FA.97/228/01"TEMP"/06 cha tarehe **06 Aprili, 2023**. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **30/07/2023** saa tisa na nusu alasiri. Maombi yote yatumwe kwa njia ya posta kwa kutumia anuani ifuatayo;-

Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya,
S.L.P. 03,
KAKONKO.

2. Dereva daraja la II – Nafasi 04

Kazi na Majukumu

- Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari.
- Kuwapeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi.
- Kufanya matengenezo madogo madogo ya gari.
- Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali.
- Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari.
- Kufanya usafi wa gari.
- Kufanya kazi nyingine kadri atakavyoelekezwa na Msimamizi wake.


Sifa za Kuajiriwa.

- Mwombaji awe na Cheti cha Kidato cha Nne Form IV au VI.
- Mwombaji awe na leseni ya Daraja E au C1 ya uendeshaji magari ambayo amefanyia kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja bila kusababisha ajali.
- Mwombaji awe amehudhuria mafunzo ya ufundi stadi (VETA) au chuo kingine kinachotambuliwa na Serikali.
- Mwombaji atakayekuwa na cheti cha majaribio ya ufundi daraja la II watafikiriwa kwanza

MASHARTI YA JUMLA

Mwombaji anatakiwa kutimiza masharti yafuatayo kikamilifu.

- (iv) Awe ni Raia wa Tanzania mwenye umri usiozidi miaka 45, bila kujali jinsi ulemavu, kabila, dini au hali.
- (v) Aambatanishe nakala ya cheti cha kuzaliwa na Maelezo Binafsi (CV) yaliyojitosheleza kwa maana ya taarifa na mawasiliano. Pia aambatanishe picha 1 "Passportsize" iliyochukuliwa hivi karibuni na nakala za vyeti vya Taaluma (Academic) na Weledi (Professional). Transcript "Testimonials" na " Provisional Results" au Statement of Results havipokelewi.
- (vi) Maombi yawasilishwe kabla au mnamo tarehe 30/07/2023 saa 9:30 Alasiri. Maombi yatakayowasilishwa baada ya tarehe na muda uliopangwa hayatafanyiwa kazi.



Ndaki S. Mhuli
MKURUGENZI MTENDAJI (W)
KAKONKO.

MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA
KAKONKO

NAKALA:-

Katibu,
Ofisi ya Rais,
Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma,
S.L.P 2320,
DODOMA.

**NB: Tangazo hili linapatikana pia kupitia tovuti ya HALMASHAURI :
www.kakonkodc.go.tz**